


UTARATIBU WA KUPANDISHA HADHI BARABARA


Imeandaliwa na:

*Kamati ya Kitaifa ya Kupanga Barabara Katika Hadhi Stahiki
(NRCC)*




Yaliyomo

1. Utangulizi
2. Sheria ya Barabara Na.13 ya mwaka 2007
3. Majukumu ya Kamati
4. Utaratibu wa Kuwasilisha Maombi ya Kupandisha Hadhi Barabara
5. Faida na Changamoto
6. Hitimisho



1.0 Utangulizi

- Utaratibu wa kupandisha au kushusha hadhi barabara upo kwa mujibu wa Kifungu cha 44(1) cha Sheria ya Barabara Na.13 ya mwaka 2007 na Kanuni za Menejimenti ya Barabara za mwaka 2009.
- Ili kukamilisha jukumu hilo Waziri mwenye dhamana ya barabara amepewa mamlaka ya kuunda Kamati ya Kitaifa ya Kupanga Barabara Katika Hadhi Stahiki (National Roads Classification Committee - NRCC).
- Jukumu kuu la kamati tajwa ni kuhakiki barabara inayoombewa kupanda hadhi, kutoa mapendekezo na kumshauri Waziri kuhusu madaraja stahiki ya barabara zilizohakikikiwa.



2.0 Sheria ya Barabara Na. 13 (2007)

Kifungu cha 12 (1) na (2); Barabara zimegawanyika katika makundi makuu mawili (2):

- i. Barabara za Kitaifa (National Roads); na
- ii. Barabara za Wilaya (District Roads).

2.1 Barabara za Kitaifa (National Roads)

- Barabara Kuu (Trunk Roads); na
- Barabara za Mikoa (Regional Roads).

Barabara hizi zinahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS).

2.2 Barabara za Wilaya (District Roads)

- Barabara za Mrisho (Feeder Roads);
- Barabara za Mkusanyo (Collector Roads); na
- Barabara za Jamii (Community Roads).

Barabara hizi zinahudumiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA).


2.0 Sheria ya Barabara Na. 13 (2007) inaendel..

Barabara Kuu:

- Barabara inayounganisha makao makuu ya mikoa miwili au zaidi;
- inayounganisha makao makuu ya mikoa na mji mkuu au mkoa wa nchi nyingine au bandari nje ya Tanzania;

Barabara za Mikoa:


- Barabara inayounganisha barabara kuu na makao makuu ya mikoa au wilaya;
- inayounganisha makao makuu ya mikoa na makao makuu ya wilaya;



2.0 Sheria ya Barabara Na. 13 (2007) inaendeleo..

Barabara za Mkusanyo (Collector Roads)

- i. Barabara inayounganisha makao makuu ya wilaya na makao makuu ya Tarafa;
- ii. Barabara inayounganisha makao makuu ya tarafa moja na nyingine;
- iii. Barabara inayounganisha makao makuu ya Tarafa na makao makuu ya Kata; na
- iv. Barabara iliyopo mjini ambayo hutumika na magari ambayo mara nyingi huanzia na kuishia nje ya mji na kuungana na barabara kuu au za mikoa.



2.0 Sheria ya Barabara Na. 13 (2007) inaendelea..

Barabara za Mrisho (Feeder Roads)


- i. Barabara iliyopo mjini inayounganisha “*collector roads*” na barabara nyingine inayopitisha magari yanayoenda viwandani, maeneo ya biashara na makazi ya watu;
- ii. Barabara ya inayounganisha makao makuu ya Kata moja na Kata nyingine;

Barabara za Jamii (Community Roads)


- i. Barabara iliyopo kijijini, ndani ya kijiji na Barabara inayounganisha kijiji na kijiji



3.0. Majukumu ya Kamati




- Kutumia vigezo vya kupandisha hadhi barabara kwa mujibu wa sheria na kumshauri ipasavyo Waziri mwenye dhamana ya barabara;
- Kuandaa semina na warsha ili kusambaza taarifa za utaratibu wa kuomba kupandisha hadhi barabara;
- Kutembelea barabara zilizoombewa kupandishwa hadhi ili kuhakiki taarifa zake kama zilivyo katika maombi yaliyowasilishwa na bodi za barabara za mikoa au mamlaka teule za barabara;
- Kuandaa taarifa, mapendekezo na ushauri kwa Mhe. Waziri mwenye dhamana ya Barabrara kuhusu upangaji wa barabara katika madaraja mbalimbali;
- Kufuatilia utekelezaji wa uamuzi wa Mhe. Waziri mwenye dhamana ya barabara kuhusu kupanga barabara katika madaraja stahiki;




4.0. Utaratibu wa Kupandishwa Hadhi Barabara

Sehemu ya 43, (1) na (2) ya Kanuni za Menejimenti ya Barabara ya mwaka 2009 inaeleza kuwa Bodi ya Barabara ya Mkoa, mtu binafsi au kikundi cha watu ndiyo wenye mamlaka ya kuwasilisha kwa Mhe. Waziri maombi ya kupandishwa hadhi barabara




4.0. Utaratibu wa Kupandishwa Hadhi Barabara

- Sehemu ya 44,(1) - (5) ya Kanuni za Menejimenti ya Barabara ya mwaka 2009 inaeleza kuwa maombi ya kupandisha hadhi barabara yawe na vitu vifuatavyo:-
 - (a) itajwe sehemu katika barabara kuu, za mikoa, feeder, collector au community inapoanzia barabara inayoombewa;
 - (b) itajwe sehemu inapoishia (*destination point*)
 - (c) Barabara inayoombewa ibainishwe:
 - i. Urefu;
 - ii. Aina ya barabara kama ni ya lami au changarawe (*type of surface and shoulders*);
 - iii. Upana wa barabara (*width of formation and carriageway*); na
 - iv. Upana wa hifadhi ya barabara.




4.0. Utaratibu waKupandishwa Hadhi Barabara

- v. Idadi na aina ya magari yanayotumia barabara hiyo;
- vi. Idadi na majina ya vijiji na miji inamopita;
- vii. Njia za mabasi (*bus routes*);
- viii. Huduma za kijamii zinazotegemea barabara hiyo mfano: soko, shule, hospitali, kliniki, kanisa na misikiti, n.k.;
- ix. Maelezo ya njia mbadala kama ipo (*alternative route*)




4.0. Utaratibu wa Kupandishwa Hadhi Barabara

- (2) Maombi yote ya kupandisha hadhi barabara yatumwe kwa Mhe. Waziri ambaye atayaelekeza kwa Kamati ya Kitaifa ya Kupanga Barabara katika Hadhi Stahiki (NRCC) ili kupata mapendekezo.
- (3) Baada ya kupokea orodha ya maombi kutoka kwa Mhe. Waziri, kamati itapitia na kuandaa taarifa ili kumshauri ipasavyo.




4.0. Utaratibu wa Kupandishwa Hadhi Barabara

- (4) akiridhia atasaini tamko la kisheria na hivyo barabara zilizokidhi vigezo zitatangazwa kwenye Gazeti la Serikali (GN).
- (5) Iwapo maombi yatakataliwa, Mhe. Waziri atamjulisha muombaji kwa maandishi akieleza vigezo na sababu za kukataliwa kwa maombi hayo.



4.0. Utaratibu wa Kupandishwa Hadhi Barabara

- (6) Iwapo barabara zilizoombewa hazijakidhi vigezo kwa mujibu wa sheria ya barabara, Waziri anaweza:
- i. Kukasimu barabara hiyo kwa mamlaka husika ili kuihudumia.
 - ii. Kuelekeza pesa itengwe katika bajeti ya Serikali kwa ajili ya barabara hiyo.
 - iii. Kuelekeza wataalam kwenda kwa mamlaka inayosimamia barabara hiyo.



4.0. Utaratibu waKupandishwa Hadhi Barabara

- (7) Mhe. Waziri ataagiza kushushwa daraja barabara ambazo hazina tena vigezo vya kuwa katika daraja lililopo sasa kwa mujibu wa sheria ya barabara.
- (8) Mtu au kikundi chochote ambacho hakitaridhika na maamuzi ya Mhe. Waziri kinaruhusiwa kukata rufaa kwa Mhe. Waziri ili maombi yapitiwe upya.
- (9) Uamuzi wa Waziri ni wa mwisho. Mamlaka husika zitajulishwa orodha ya Barabara zitakazokuwa zimepandishwa madaraja. Pesa za Mfuko wa Barabara zitapangwa kulingana na mabadiliko hayo..


5.0 Faida na Changamoto

Faida:

- Barabara kupangiwa fedha za mfuko wa barabara na kuhudumiwa na mamlaka husika;

Changamoto:

- Kuongezeka kwa eneo la hifadhi ya barabara kutokana na kupanda hadhi. Hivyo Serikali kutakiwa kulipa fidia kwa nyumba na mali zitakazohusika;
- Kuongezeka kwa mahitaji ya rasilimali fedha ili kuhudumia barabara zilizohusika; na
- Kupungua kwa idadi ya barabara nzuri na hivyo kupungua kwa huduma bora za usafiri wa barabara kijamii kwa barabara zilizoshushwa hadhi kwakuwa zitapata fedha pungufu.



ASANTENI